



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA  
SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA  
KAHAMA.**



**Kumb.Na.KMC/F.20/10/72**

**30 Juni, 2023**

## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MKATABA**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama anapenda kuwatangazia Wananchi wote wenye sifa, nafasi Arobaini (40) za Ajira ya Mkataba ya wakusanya Mapato katika Halmashauri ya Manispaa Kahama.

### **SIFA ZA MWOMBAJI**

- i. Mwombaji awe Raia wa Tanzania.
- ii. Awe amehitimu Kidato cha Nne na kuwa na ufaulu wa Daraja la Nne.
- iii. Awe na Mdhamini mwenye Makazi yake Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mwenye mali isiyohamishika.
- iv. Awe Mwadilifu na ambaye hajawahi kukutwa na hatia Mahakamani.
- v. Awe na uwezo wa kufanya kazi kwa kujituma bila kusimamiwa.
- vi. Awe tayari kufanya Kazi katika Kata yeyote kwa kipindi kisichopungua Mwaka Mmoja.
- vii. Awe na uzoefu wa kukusanya Mapato wenye historia nzuri kwa kipindi kisichopungua Mwaka Mmoja.
- viii. Awe na Umri wa kuanzia Miaka 18 hadi 35.
- ix. Kipaumbele pia atapewa anayefahamu kuendesha Pikipiki.

## KAZI NA MAJUKUMU


1. Kukusanya Mapato ya Halmashauri ya Manispaa Kahama

### MAMBO YA JUMLA YA KUZINGATIA.

- i. Nakala ya Cheti cha Kidato cha Nne.
- ii. Waombaji waambatishe vivuli vya Vyeti vya Elimu, maelezo binafsi (CV), Nakala ya Cheti cha kuzaliwa.
- iii. Katika barua ya maombi, weka Namba yako ya simu inayopatikana muda wote.
- iv. Barua zibandikwe picha mbili (2) - Passport size.
- v. Waombaji watakaokidhi sifa na vigezo watajulishwa tarehe ya usaili.
- vi. Maombi yote yaambatane na barua za Wadhamini watatu zinazoonesha Mali zisizohamishika.
- vii. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **13/07/2023** saa **9:30** alasiri.
- viii. Maombi yote yaelekezwe Ofisi ya Mkurugenzi Manispaa ya Kahama kwa Anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Manispaa,  
Barabara ya Boma,  
S.L.P 472,  
**KAHAMA**

Limetolewa na:

  
Anderson D. Msumba.  
**MKURUGENZI.**  
**HALMASHAURI YA MANISPAA**  
**KAHAMA.**

MUNICIPAL DIRECTOR  
KAHAMA MUNICIPAL  
P.O. Box 472  
KAHAMA